

**JAMHURI YA MUUNGANO WATANZANIA  
OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA WILAYA YA MPWAPWA  
Barua zote ziandikwe kwa Mkurugenzi Mtendaji (W)**



Unapojuji Tafadhali Taja:-  
Kumb.Na.HW/MPW/S10/51 VOL I/109

S.L.P 12,  
**MPWAPWA.**  
26.03.2018

## **TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI**

### **1. UTANGULIZI.**

Mkurugenzi mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa anapenda kuwatangazia nafasi za kazi watanzania wenyewe sifa na uwezo wa kujaza nafasi za kazi za watendaji wa vijiji kwa masharti ya kudumu. Tangazo hili ni baada ya kupokea tangazo la ajiri mbadala chenye **Kumb. Na. CFC 26/205/01 "F" c/91** ha tarehe **22/08/2017** pamoja na barua ya nyongeza ya muda wa utekelezaji kibali cha ajiri mbadalakwa watendaji wa vijiji na mitaa yenye **Kumbu Na CFC.26/205/01/ "GG" /95** ya tarehe **12,Machi,2018** zote kutoka kwa katibu Mkuu Utumishi. Mchanganuo wa nafasi ni kama ifuatavyo:-

### **2.0 WATENDAJI WA VIJIFI- III NAFASI- AROBAINI NA NNE (44).**

#### **2.1 SIFA**

**Mwenye Elimu ya kidato cha Nne (IV) Au Sita (VI) aliyehitimu mafunzo ya Astashahada/ Certificate/ " Technician Certificate"** katika moja ya fani zifuatazo:-

Utawala, Sheria, Sayansi ya jamii, Usimamizi wa fedha, Maendeleo ya jamii na Sayansi ya sanaa kutoka katika chuo cha serikali za Mitaa Hombolo, Dodoma au chuo chochote kinachotambuliwa na serikali.

#### **2.2 MAJUKUMU**

- Afisa masuuli na Mtendaji Mkuu wa Serikali ya Kijiji.
- Kusimamia Ulinzi na Usalama wa raia na mali zao,kuwa mlinzi wa amani na msimamizi wa Utawala Bora katika Kijiji.
- Kuratibu na kusimamia upangaji wa utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo ya kijiji.
- Katibu wa mikutano na kamati zote za halmashauri ya kijiji.
- Kutafsiri na kusimamia Sera, Sheria na Taratibu.
- Kuaanda taarifa za utekelezaji wa kazi katika eneo lake na kuhamasisha wananchi katika kuanda na kutekeleza mikakati ya kuondoa njaa, umaskini na kuongeza uzalishaji mali.
- Kiongozi wa wakuu wa vitengo vya kitaalamu katika kijiji.
- Kusimamia,kukusanya na kuhifadhi kumbukumbu zote na nyaraka za kijiji.
- Mwenyekiti wa kikao cha wataalamu waliopo katika kijiji.
- Kupokea ,kusikiliza na kutatua malalamiko na migogoro ya wananchi.
- Kusimamia utungaji wa sheria ndogo za kijiji na
- Atawajibika kwa Mtendaji wa kata.

### **2.3 MSHAHARA.**

Kwa kuzingatia viwango vya Serikali Ngazi ya mshahara itakuwa **TGS B. (390,000=)** kwa Mwezi.

### **3.0 MAELEZO/ MASHARTI YA JUMLA**

- i. Mwombaji awe raia wa Tanzania na awe tayari kufanya kazi sehemu yeyote katika Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa
- ii. Mwombaji awe na umri kati ya miaka 18 na usiozidi ya miaka 45 na awe hajawahi kupatikana na kosa la jina au kufungwa jela.
- iii. maombi yote ya waombaji waambatanishe maelezo binafsi yaliyojitosheleza (Curriculum Vitae ) namba ya simu na anuani sahihi, barua pepe (e-mail address) na majina ya wadhamini (referees) watatu wanaofahamika.
- iv. Waombaji lazima waambatanishe nakala za vyeti vifuatavyo:-
  - a) Astashahada/cheti cha utaalamu kulingana na Sifa za nafasi husika.
  - b) Cheti cha kidato cha nne au sita.
  - c) Cheti cha kuzaliwa.
  - d) Na picha mbili za rangi za hivi karibuni (passport size) na iandikwe jina nyuma
- v. Matokeo ya muda - provisional/testimonials/statement of results, hati ya matokeo ya kidato cha nne na sita havitakubaliwa.
- vi. Waombaji wawe wenye sifa zilizotajwa kwenye tangazo hili la kazi.
- vii. Waajiriwa wa serikali maombi ya barua yapitie kwa waajiri wao.
- viii. Waombaji watakaoleta maombi na vyeti vya kugushi hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi yao.
- ix. Waombaji wa makundi maalumu wanashawishiwa kuomba.
- x. Waombaji wenye vyeti vya kidato cha nne na sita vya nje ya nchi vitatakiwa vithibitishwe na NACTE.
- xi. Waombaji wenye vyeti vya astashahada ya nje ya nchi vithibitishwe na TCU na taarifa ya uhakiki iambatanishwe .
- xii. Barua ya maombi itatakiwa iandikwe kwa Kiswahili au Kiingereza na iandikwe kwa mkono.
- xiii. Siku ya usaili kila mwombaji afike ~~na~~ passport size 2 vyeti halisi vya Elimu,Taaluma na kuzaliwa.
- xiv. **Mwisho wa kupokea barua za maombi ni Jumatano, tarehe 08/04/2018 saa 9:30 alasiri.**


Maombi yote yatumwe kwa:-

**Mkurugenzi Mtendaji (W),  
Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa,  
S.L.P 12,  
MPWAPWA.**

Imetolewa na

  
Mohamed A. Maji

**MKURUGENZI MTENDAJI,  
HALMASHAURI YA WILAYA YA MPWAPWA.**

  
MKURUNGEZI MTENDAJI (W)  
HALMASHAURI YA WILAYA  
S. L. P. 12  
MPWAPWA